# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA WAZIRI MKUU
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**MKOA WA MARA**
**Anuani ya simu "Admin"**
**Simu ya mdomo: 028-2690045**
**Barua pepe:das.tarime@mara.go.tz**
**Unapojibu tafadhali taja:**
**Kumb: Na.AB.95/207/01A/20**

**OFISI YA MKUU WA WILAYA,**
**8 BARABARA YA UTAWALA,**
**S. L. P. 1,**
**31481 TARIME-MARA.**

**22/01/2026**

# TANGAZO! TANGAZO! TANGAZO!

## YAH: UANDIKISHAJI WA VIJANA KUJIUNGA NA JESHI LA KUJENGA TAIFA KWA UTARATIBU WA KUJITOLEA (HIARI) MWAKA 2025/2026

**TAREHE YA TANGAZO: 22/01/2026**

Mkuu wa Wilaya ya Tarime anawatangazia wananchi wa Wilaya ya Tarime nafasi za uandikishwaji wa vijana wa hiari kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) mwaka 2025/2026.

**SIFA ZA MWOMBAJI**:

1. Awe raia wa Tanzania.
2. **Umri:**
   a. Kwa vijana wenye Elimu ya darasa la saba umri ni kuanzia miaka 16 hadi 18 waliomaliza Elimu ya msingi kuanzia mwaka 2022, 2023, 2024, 2025 na awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Msingi.

   b. Vijana wenye Elimu ya kidato cha nne umri usiwe Zaidi ya miaka 20, waliomaliza Elimu ya Sekondari kuanzia mwaka 2022, 2023, 2024, 2025 na awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Sekodnari (Secondary Leaving Certificate) na cheti halisi cha matokeo (Academic Certificate). Awe na ufaulu wa daraja la kwanza hadi daraja la nne. Kijana mwenye daraja la nne awe na ufaulu wa Alama kuanzia 26 hadi 32.

   c. Vijana wenye Elimu ya kidato cha sita umri usiwe Zaidi ya miaka 22, waliomaliza Elimu ya Sekondari kuanzia mwaka

2022, 2023, 2024, 2025 na awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Sekondari (Secondary Leaving Certificate) na cheti halisi cha matokeo (Academic Certificate). Awe na ufaulu wa kuanzia daraja la kwanza hadi daraja la nne.

d. Vijana wenye Elimu ya Stashahada umri usiwe Zaidi ya miaka 25, awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo.

e. Vijana wenye Elimu ya Shahada umri usiwe Zaidi ya miaka 26, awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha chuo.

f. Vijana wenye Elimu ya Shahada ya uzamili umri usiwe Zaidi ya miaka 27, awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo.

3. Awe na Afya njema, Akili timamu na asiwe na alama yoyote ya michoro mwilini (Tattoo).

4. Mwenye tabia na nidhamu nzuri, hajapatikana na hatia Mahakamani na hajawahi kufungwa.

5. Awe na kitambulisho cha Taifa au namba ya utambulisho kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

6. Awe na cheti halisi cha kuzaliwa (Original Birth Certificate).

7. Asiwe ametumikia Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo au Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo wala kuajiriwa na Idara nyingine Serikalini.

8. Asiwe amepitia JKT Operesheni za nyuma kwa kundi la kujitolea au kundi la lazima (Mujibu wa Sheria).

9. Asiwe amejihusisha na matumizi ya madawa ya kulevya, bangi na yanayofanana na hayo.

10. **ANGALIZO**:
    i. Kijana atakayepatikana na nyaraka za kughushi atachukuliwa hatua kali za kisheria kulingana na taratibu zilizopo.

    ii. Maombi yaandikwe kwa mkono na kutumwa kwa anuani ifuatayo;

***Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,***
***8 Barabara ya Utawala,***
***S.L.P 1,***
***31481 TARIME.***

iii. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **26/01/2026** saa 9.30 Alasiri. Maombi yanapokelewa Ofisi ya Mshauri wa Jeshi la Akiba Wilaya ya Tarime iliyopo mkabala na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Tarime, kwa njia ya mkono.

***RUSHWA NI ADUI WA HAKI.***

***Martha O. Gagiri***
Kny:KATIBU TAWALA WILAYA
**TARIME**

KATIBU TAWALA WILAYA
TARIME.